



Twafahamu kuwa
Tembo ana mkonga
mrefu.



Zamani, pua la Tembo
lilikuwa fupi na nono.
Pua hilo lilionekana
kama kiatu
kilichopachikwa
katikati ya uso wake.




Siku moja, Tembo alizaa mtoto aliyekuwa mdadisi sana.


Alimwuliza swali kila mnyama aliyemuona.




Mtoto wa Tembo
alimdadisi Twiga, "Kwa
nini shingo yako ni
ndefu?"




Pia alimdadisi Kifaru,
"Kwa nini pembe yako
ina ncha iliyochongoka
sana?"



Mtoto wa Tembo pia alimdadisi Kiboko, "Kwa nini una macho mekundu?"




Alipomwona Mamba,
alimdadisi, "Wewe
hula nini?"



Mamake alimwonya,
"Mwanangu,
usiwaulize wanyama
maswali kama hayo?"
Mtoto wa Tembo
alinuna akaenda
kucheza.



Kunguru mwerevu
akamwambia Mtoto
wa Tembo, "Nifuate
twende mtoni
nikuonyeshe
wanachokula
mamba."



Mtoto wa Tembo
akamfuata Kunguru
hadi mtoni.



Alijipenyeza katikati ya mianzi kwenye ukingo wa mto. Akatazama majini kisha akauliza, "Mamba mwenyewe yuko wapi?"



Jiwe lililokuwa karibu
na mto lilisema,
"Hujambo?"
"Sijambo," alijibu
Mtoto wa Tembo.
"Unaweza kunieleza
wanachokula mamba
jioni?"



Jiwe lilimjibu, "Hebu inama kidogo nikwambie wanachokula mamba." Mtoto wa Tembo aliinama chini karibu kabisa na lile jiwe.



Wakati huo huo pua la Mtoto wa Tembo lilikuwa kinywani mwa mamba. "Mamba ataila nyama yako leo," Kunguru mjanja akasema.




Mtoto wa Tembo akakita chini miguu yake yenye nguvu, akasimama imara akaanza kujivuta. Mamba hakuliachilia pua la Mtoto wa Tembo.




Pua la Mtoto wa
Tembo likarefuka zaidi,
kisha, puu! Mtoto wa
Tembo akaanguka
kichalichali.



Baada ya kukikosa
chakula chake, mamba
alizama na kutokomea
majini.



Mtoto wa Tembo
alilitazama pua lake.
Lilikuwa refu kama
mkonga na hakuweza
kuona lilipoishia.



Mkonga wake mrefu
ulimwezesha kuchuma
matunda yaliyokuwa
kwenye matawi ya juu.



Pia, aliweza kuoga
wakati wa joto
kuutumia mkonga ule.